MAMLAKA YA MAFUNZO NA UFUNDI STADI (VETA)

1.**Swali:** Tupe historia fupi ya VETA.

Jibu: Historia ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inaanzia mwaka 1940 tulipokuwa na sheria ya kusimamia mafunzo viwandani (Apprenticeship Ordinance). Mwaka 1974 sheria hiyo ilifutwa na badala yake ikapitishwa Sheria ya Mafunzo ya Ufundi Stadi ya 1974 ambayo iliunda Idara ya Mafunzo ya Ufundi Stadi chini ya Wizara ya Kazi. Ilipofika mwaka 1994 sheria ilibadilishwa tena ambapo Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilipitishwa na Bunge. Hii ndiyo sheria iliyoanziasha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

2.**Swali:** Madhumuni ya kuanzishwa kwa VETA ni yapi?

Jibu: Madhumuni ya kuanzishwa kwa VETA ni kama yafuatayo:

a) Kutoa fursa na miundombinu ya mafunzo ya ufundi stadi
b) Kuanzisha mfumo wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kukidhi mahitaji ya sekta isiyo rasmi na sekta rasmi
c) Kukidhi mahitaji ya soko la ajira kwa kuwapatia wafanyakazi stadi za kazi ili kuongeza uzalishaji na tija katika uchumi.
d) Kuhakikisha kuwa mfumo wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi unazingatia mahitaji, unapunguza gharama na hatua kwa hatua mikoa inapewa mamlaka katika kupanga na kutekeleza ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na mafunzo yanayotolewa.
e) Kukuza na kuendeleza ujasiriamali kama sehemu ya mafunzo yanayotolewa.
f) Kuendeleza mafunzo katika sehemu za kazi.
g) Kuendeleza mazingira ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa makundi yaliyosahaulika.
h) Kutafuta fedha na kugharimia elimu na mafunzo ya ufundi stadi
i) Kuongeza ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa
j) Kuendeleza au kutoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanayotokana na mahitaji kwa kuzingatia mipango ya maendeleo na sera za taifa.

3.**Swali:** Mmepata mafanikio gani katika kipindi cha miaka 10 iliyopita?

Jibu: VETA, kwa kushirikiana na wadau wote imetoa miongozo ya mafunzo ya stadi za kazi, stadi za maisha na stadi za kujinusuru. Miongozo hii imewezesha kuwepo kwa mtandao wa vyuo vya ufundi stadi chini ya VETA na vya watu binafsi vinavyotoa mafunzo kwa vijana ambayo yamewezesha vijana kupata stadi za kuweza kujiajiri na kupamabana na umaskini. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika miaka kumi iliyopita (1995-2005) ni kama ifutavyo:

i) VETA imekamilisha ujenzi wa vyuo vinne vya ufundi stadi vya mikoa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Mtwara na Kigoma. Sasa imeanza ujenzi wa vyuo vingine vitatu vya ufundi stadi vilivyobakia katika mikoa ya Pwani, Lindi na Manyara. Hii inakamilisha azma ya serikali ya kuwa na chuo cha ufundi stadi cha mkoa katika kila mkoa.

ii) Idadi ya vijana wanaojiunga na mafunzo katika stadi mbalimbali katika vyuo vya VETA na vile vinavyoendeshwa na serikali (Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDCs) kwa mwaka imeongezeka kutoka 3670 mwaka 1995 kufikia 41,880 mwaka 2004. katika kozi ndefu na fupi.

iii) Vyuo vya watu binafsi na asasi zisizo za kiserikali navyo vimeongeza idadi ya wanafunzi kwa mwaka kutoka 35,490 mwaka 1995 kufikia 55,265 mwaka 2004 katika kozi ndefu na fupifupi. Ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji uliofanywa na VETA ambapo sekta binafsi inapaswa kuwa mstari wa mbele katika uwekezaji katika ufundi stadi.

iv) Jumla ya vyuo vinavyotoa mafunzo ya stadi za kazi vilivyosajiliwa na VETA vimeongezeka kutoka 330 mwaka 1995 kufikia 764 mwaka 2004. Ni jukumu la VETA kuhakikisha vyuo vinatoa mafunzo bora ya ufundi stadi. Ongezeko hilo linaonyesha kuwa vyuo vinavyotoa mafunzo bora vimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 50.

v) Idadi ya wasichana wanaoshiriki katika mafunzo ya stadi za kazi mbalimbali imeongezeka kutoka 12% mwaka 1995 kufikia 32% mwaka 2004. VETA imeweza kuhamasisha wasichana wajiunge na mafunzo katika fani ambazo zinatawaliwa na wanaume kama vile umeme, ufundi magari, uashi, ufundi bomba n.k.

vi) Fani za mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa na vyuo vya VETA, vile vinavyoendeshwa na serikali pamoja na vile vinavyomilikiwa na watu binafsi na asasi zisizo za kiserikali zimeongezeka kutoka 36 mwaka 1995 kufikia 93 mwaka 2004. Ongezeko hilo limetokana na mahitaji ya soko la ajira.

4.**Swali:** Mnatoa kozi za aina gani?- Aidha kozi za muda mfupi huchukua wastani wa muda gani na kozi ndefu kabisa zinachukuwa muda gani?

Jibu: Vyuo vya ufundi stadi vinatoa mafunzo ya stadi za kazi katika sekta mbalimbali kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Kozi za muda mfupi huanzia wiki moja hadi miezi 6. Kozi ndefu huchukua muda wa zaidi ya miezi sita hadi miaka miwili.

5.**Swali:** Mnatekeleza vipi mipango ya Serikali ya kupambana na umasikini kwa kutokomeza ukosefu wa ajira kwa vijana kupitia kozi zenu?.

Jibu: VETA imehusishwa kikamilifu na serikali katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Katika kutekeleza mpango huo,VETA inatoa mafunzo ya stadi za kazi ili kuwawezesha waliohitimu kuajiriwa ama kujiajiri katika sekta isiyo rasmi. Mkazo mkubwa unatolewa katika kumwezesha mhitimu kujiajiri mwenyewe kwa kupewa stadi za ujasiriamali pamoja na stadi za kazi. Kutokana na mafunzo yanayotolewa vijana wameweza kuanzisha miradi mbalimbali katika fani za useremala, ufundi magari, umeme, uashi, uundaji vifaa n.k. Vijana ambao wameajiajiri pia wameajiri vijana wengine katika miradi yao . Hivyo VETA imeweza kutoa mchango katika kupambana na umaskini na kutokomeza tatizo la ajira.

6.**Swali:** Je mnavyo vituo(vyuo) vingapi vya mafunzo kwa nchi nzima na viko katika mikoa gani?

Jibu: VETA inamiliki na kuendesha vyuo vya ufundi stadi 20 katika mikoa 17 ya Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Singida, Tabora, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Kilimanjaro, Tanga na Arusha. VETA pia imekamilisha ujenzi

wa chuo katika mkoa wa Kigoma na mafunzo yataanza kutolewa hivi karibuni.

Pia VETA inamiliki na kuendesha Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro ambacho kinatoa mafunzo ya ualimu kwa ajili ya vyuo vya ufundi stadi nchini.

VETA inasimamia na kuratibu mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vingine zaidi ya 840 nchini kote. Vyuo hivi vipo katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara.

7.**Swali**: Tueleze mafanikio na matarajio yenu ya baadaye

Jibu: Kama tulivyoeleza hapo juu VETA imepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Tunayo matarajio makubwa ya baadaye.

Hivi sasa mchakato wa kuandaa mpango wa miaka 5 (2006-2010) unaendelea vizuri ambapo tunahusisha wadau wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Matarajio yetu ni kwamba ifikapo mwaka 2010, VETA iwe inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko hivi sasa katika kutoa stadi zinazohitajika katika sekta isiyo rasmi na hivyo kupiga vita umasikini. Hali kadhalika iwe na uwezo wa kuchangia zaidi katika kutoa mafunzo kwa stadi zinazotakiwa katika sekta rasmi na hivyo kuongeza pato la taifa.

Mambo muhimu yatakayozingatiwa katika miaka mitano ijayo ni:

i. Mafunzo yanayotolewa yaendane na mahitaji ya sekta zote mbili, rasmi na ile isiyo rasmi.

ii. Kuboresha zana za kufundishia (tools and equipment) ili mafunzo yanayotolewa yawe bora zaidi kulingana na viwango vya kitaifa.

iii. Kutekeleza mpango kabambe wa kutoa mafunzo kwa waalimu wa ufundi stadi ili waende sambamba na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea.

iv. Kutanua nafasi za mafunzo ya ufundi stadi kulingana na upanuzi unaotokea katika elimu ya msingi na sekondari, ambao utaongeza idadi ya wanafunzi watakaojiunga na mafunzo hayo.